

# MIUNGANISHO

Aprili 14, 2022

## KONA YA MSIMAMIZI

Jambo jumuiya yetu ya PPSD, na karibu kwenye toleo la pili la jarida letu la kila wiki. Ukikosa matoleo yeyote ya jarida hili, unaweza kuyapata hapa kwenye tovuti ya Wilaya kwa lugha nyingi. Lengo letu ni kukupa masasisho thabiti kuhusu habari za PPSD, kusherekea mafanikio ya wanafunzi, kukutambulisha baadhi ya wafanyakazi wetu wazuri na kukujulisha kuhusu mikutano na matukio zijazo.


Tuna wiki chache tu ndani ya Aprili na tayari ni mwezi kweli! Kama umeskia, wiki iliyopita nilipata tuzo ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa kudumu na Gavana McKee na Kamishana Infante-Green. Tafadhali fahamu kuwa wanafunzi wetu watakuja kwanza katika kila uamuzi ninaofanya, na Mpango ya Hatua ya Mabadiliko uliyotayarishwa na jumuiya yetu utakuwa Nyota yangu ya Kaskazini tunapofanya kazi pamoja kugeuza Providence kuwa mahali pa elimu.

Kama mkuu wa zamani na msaidizi mkuu hapa PPSD, najua kwamba lazima tuwe na uhusiano thabiti dhidhi ya ofisi yetu kuu na shule zetu. Hii ni juhudi ya timu kusaidia wanafunzi wetu kufaulu! Kwa hivyo katika wiki kadhaa zilizopita nimeifanya iwe lengo langu kutembelea kila shule binafsi ili kuzungumza na wanafunzi, wafanyakazi na wakuu wa shule ili kujifunza jinsi tunavyoweza kusaidiana vyema zaidi. Ninahimiza yeyote anayesoma jarida hili kujihusisha katika mazungumzo hayo kwa kuwasiliana na communications@ppsd.org. Sauti zenu ni muhimu, na zitaheshimiwa kila wakati katika ofisi yangu!



DR. JAVIER MONTAÑEZ
Msimamizi

## MASASISHO YA WILAYA



### SERA YA SHULE YA BARAKOA

Barakoa sasa ni kwa hiari kwa wanafunzi na wafanyakazi kwa shule za Providence. Uamuzi huu ulifikiwa baada ya mazungumzo ya kina na idara ya Afya na Ride, na uchunguzi wa kina wa viwango vya kesi za COVID kote Wilayani. Kwa muda wa wiki kadhaa zilizopita, PPSD imekuwa na wastani wa kesi chini ya kumi kwa siku katika wilaya za zaidi ya wanafunzi 20,000.

Tafadhali kumbuka kuwa barakoa ni tu safu moja ya mkakati wa Wilaya wa kukabiliana na COVID. Wilaya itaendelea kutoa zahanati za chanjo bila malipo, upimwaji wa haraka bila malipo, ongezeko la usafishaji hewa shuleni na kuongezeka kwa usafi wa mazingira. Barakoa zinaweza kuhitajika tena katika baadhi ya shule au shule zote ikiwa kuna ongezeko katika visa. Maoni hasi kuhusu chagua la barakoa ya mtu yeyote hayatavumiliwa.

Tafadhali bofya hapa ili upate miongozo kamili ya kutumia barakoa ambayo ilitangazwa Aprili 6.

### LIKIZO YA APRILI

**Wanafunzi wote na wafanyakazi wote watarudi kutoka likizo la Aprili siku ya jumatatu, Aprili 25.** Hakutakuwa na kurudi polepole kwa mapumziko kama vile likizo za shule za awali. Mapumziko ya Aprili huanza Aprili 18 hadi 22.


Marejeo ya kawaida kutoka kwa likizo ya Aprili huonyesha kupungua kwa visa vya COVID 19 kote Wilayani, na usumbufu mdogo wa maandalizi ya upimaji wa mfumo wa Tathmini ya kina wa Kisiwa cha Rhode (RICAS)

### UPIMAJI WA COVID

Wilaya kwa mara nyingine tena itawapa wanafunzi wote vifaa vya kupima COVID-19 nyumbani bila malipo kabla ya likizo ya shule. Upimaji nyumbani itasambazwa kwa wanafunzi na wazazi mnamo Aprili 13 na 14. Familia zinapaswa kufuata maagizo yaliojumuishwa katika kisanduku cha kufanya majaribio ya nyumbani siku moja kabla ya wanafunzi wao kurudi shuleni kutoka likizo. Wanafunzi ambao wamepatikana na virusi lazima wajitenge kwa siku tano na wazazi wanapaswa kuripoti habari hiyo kwa shule ya mtoto wao. Wanafunzi wote walio na fomu za idhini pia watapimwa watakaporejea shuleni jumatatu Aprili 25.

## KUWASHANGILIA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo ya ajabu kila siku! Hapa kuna mifano kadhaa.





### UJUZI MAREKANI

Hongera kwa wote walioshiriki **Ujuzi Marekani 2022 Michuano ya Jimbo** mwaka huu! Wanafunzi wa PPSD walipokea **medali 18 za dhahabu** katika mashindano kama Utayarishaji wa Televisheni, Hotuba Iliyotayarishwa, Chuma, Upishi wa Kitamaduni na zaidi. Mashindano yao ya ujuzi yalifanyika kuanzia Machi 4 hadi Machi 30 na wanafunzi wakishindana na shule nyingine za Rhode Island. Washindi wa medali ya dhahabu wataendelea na mashindano ya kitaifa huko Atlanta.

*Picha ya kushoto: Mwanafunzi wa PCTA Fritz Heitmueller, kushoto, mshindi wa fedha, mwalimu David Santos, na Naomi Felix Monanci, Mshindi wa medali ya dhahabu katika Sekta ya Viwanda katika injini usukani.*


*Picha ya Kulia: Mwanafunzi wa PCTA Melvin Coc Orella, Orellana, mshindi wa medali ya Dhahabu katika upishi, katikati pamoja na Wakufunzi wa upishi Krista Taft na Johandry Rodrigues.*



### BIOLOJIA YA DAWA KWA HOSA


**Timu ya JSEC la daraja la 9 ya Biolojia ya Dawa** ziling'ara **katika** kongamano la Uongozi la Jimbo la Rhode Island HOSA ziliposhindana na timu 150 za RI. Hongera kwa wanafunzi wetu wote walioshiriki na pongezi kubwa kwa timu iliyoshiriki nafasi ya tatu.

HOSA ni shirika la kimataifa linaloongoza na wanafunzi linatambuliwa na Idara ya Elimu ya Marekani na Idara ya Afya na huduma za kibinadamu na mashirika kadhaa ya serikali na Jimbo. Dhamira yao ni kuwawezesha Watalamu wa afya wa HOSA- siku za baadaye kuwa viongozi katika jumuiya ya afya duniani, kupatia elimu, ushirikiano na uzoefu.



### WAPISHI WAJAO

**Shindano la Wapishi Wajao** la maadhimisho ya miaka 10 ya Sodexo lilifanyika Aprili 2 katika Shule ya Providence ya Kazi na Kiufundi! Wahitimu wa daraja la 5 waliwasilisha ubunifu wao kwa mjumbe wa Bodi ya Shule Ty'Relle Stephens, Mkuu wa Uendeshaji wa PPSD Salvador Pellerano, na Mpishi Derek Wagner wa Nick Kwenye Broadway. Hongera kwa Mpishi Ajaye, Jenaya, kwa picha juu, wa **Shule ya Msingi ya Mtaa wa Veazie**!





## ANGAZA WAFANYAKAZI

Jua watu wa ajabu wanaofanya kazi na wanafunzi wetu kila siku!

**Katherine Gonzalez, M.Ed**

*Mkufunzi katika Kituo cha Sherlock kuhusu Ulemavu katika RIC*

*Mwalimu wa Elimu Maalum ESC*

Iliyo katika: Shule ya Upili ya Mount Pleasant

Alijiunga na PPSD mnamo: 2012

**Je, unaeza kuelezeaje kazi yako kwa rafiki ambaye hajui mengi kuhusu elimu?**
Ninaanza kwa kueleza kwamba sisi sote tuna uwezo wa kujifunza – baadhi yetu tunaifanya tofauti. Na kazi yangu ni kuwasaidia wanafunzi kutafuta njia wanazojifunza vyema zaidi. Kwa sasa ninafanya kazi na darasa la elimu maalum la wanafunzi 11 wa mwaka wa pili huko Mount Pleasant, na ninatoa usaidizi kwa wanafunzi 11 wa ziada nje ya darasa hilo. Wanafunzi wana mahitaji anuwai ikiwa ni pamoja na ulemavu wa akili, tawahudi, na kupooza kwa ubongo. Kwa hivyo kazi yangu ni kuzingatia mahitaji yao, kuwatia moyo na kuwaonyesha huruma.

**Ni sehemu gani bora kwa kazi yako?**
Wanafunzi wangu! Hao ni fahari na furaha yangu. Na uwiano ninayojenga nao sio tu ya ajabu kwa kiwango cha kibinafsi – wana matokeo ya kweli darasani. Nimekuwa nikisoma Mafunzo ya Kihisia ya Kijamii kwa miaka kadhaa iliyopita, na ninaweza kukuambia kabisa kwamba kujenga uhusiano na kuchukua muda wa kusikiliza wanafunzi huweka hatua kwa kila kitu kingine. Nina usumbufu mdogo darasani sasa, na watoto ambao walikuwa wakiangaika wanastawi.

**Je, ni changamoto gani ambayo wewe au mmoja wa wanafunzi wako ameshinda mwaka huu?**
Mwaka jana nilipokutana na kundi hili la watoto, changamoto kubwa ilikuwa mahitaji yao ya kihisia na kijamii na kujenga uhusiano baada ya kuwa nje ya shule kwa muda mrefu kwa sababu ya COVID. Lakini sasa wanafanya vizuri zaidi kujaliana. Baadhi ya wanafunzi wamepiga hatua kubwa katika afya ya Kihisia ya Kijamii, na hiyo inasaidia kuleta wanafunzi wengine pia. Wanauliza kuhusu marafiki zao ikiwa wamekosa siku moja ya darasa, na wanasaidia katika kufanya kazi zao.

> Wanafunzi wangu… ni fahari na furaha yangu. Na uwiano ninayojenga nao sio tu ya ajabu kwa kiwango cha kibinafsi – wana matokeo ya kweli darasani.


## NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- Klabu ya Usafishaji ya Shule: 'Kuhifadhi mazingira kipande kimoja cha chakula kwa wakati mmoja'
  Jarida la Providence, Aprili 4, 2022
- Shule ya Msingi ya D' Abate itakarabatiwa kwa na milioni $21 msimu huu wa joto
  Jarida la Providence, 1 Aprili 2022
- Wanafunzi wa Providence wanaovaa barakoa watawasiliana na kaimu mkuu kupitia barua
  NBC, 10 HABARI, Aprili 1, 2022
- Escuelas Públicas de Providence buscan conocer opinión de padres sobre el uso de mascarillas
  Telemundo, March 30, 2022
- Mwanafunzi wa Shule ya Upili ya Providence ashinda Shindano la Ushairi la Jimbo
  Patch, Machi 31, 2022

## WEKA ALAMA KWENYE KALENDA ZAKO!


- **KADI ZA RIPOTI**
  *Ilichapishwa katika Skyward*
  Alhamisi, Aprili 14, 2022
- **IJUMAA KUU**
  Ijumaa, Aprili 15, 2022
  ***Hakuna Shule***
- **MAPUMZIKO YA MASIKA**
  Aprili 18, 2022 - Aprili 22, 2022
- **MKUTANO WA BODI YA SHULE**
  Jumatano, Aprili 27, 2022 6.30 mchana.
  797 Westminster Street, 3rd fl, Providence

## SAMBAZA NENO




### PVDFEST

**PVDFest** itaandaa **Youth Stage** kwa vijana wasanii katika tamasha la mwaka huu! Ombi zimefunguliwa! Tembelea https://pvdfest.com/perform/ kuwasilisha ombi lako.




### KAZI ZA VIJANA

Maombi ya **nafasi za kazi za vijana** na Idara za Mbuga na Burudani za Jiji sasa yamefunguliwa → pata maelezo zaidi: http://pvdsummerjobs.com

Providence Schools EARLY CHILDHOOD PROGRAM

### RI PRE-K

Bahati na sibu ya mwaka wa **2022-2023 ya programu ya RI Pre-K** imefunguliwa. RI Pre-K, inatoa bure, elimu ya Pre-K ya ubora wa juu kwa watoto wanaohitimu wenye umri wa miaka 4 kote Rhode Island. Pata maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kutuma ombi: http://www3.ride.ri.gov/pklottery

Mambo ya kusisimua yanatokea Wilaya nzima, na tunataka kutangaza! Ikiwa una programu, tukio, mfanyakazi au mwanafunzi aliye na hadithi ya kupendeza ambayo ungependa kuangazia, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.

Providence Schools

© 2022 Shule za Umma za Providence · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org